# AMIN YA MAHMOOD

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

# Amin ya Mahmood

Tafsiri ya Kiswahili ya: Mahmood ki Amin (Kiurdu)

**Mahmood ki Aameen** (Swahili Translation)

**Mwandishi:**
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

**Mfasiri:**
Jamil R. Rafiq

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1897
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2021

© Islam International Publications Ltd.

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

**ISBN:** 978-1-84880-783-9
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا اِنَّكَ اَنْتَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ

# محمود کی آمین

سنہ ۱۳۱۹

جسکو

ڈاکٹر عباد اللہ ایم بی نے مطبع البشیر ہند ہال بازار
امرتسر میں طبع کرایا
بار ثانی

Ee Mola wetu, Utupokelee, hakika Wewe ndiwe Mwenye kusikia Mwenye kujua.

# AMIN YA MAHMOOD

1319 Hijri

Ambayo

Alichapisha Dk. Ibadullah, M.A., ndani ya Matbaa Bashir Hind, Hal Bazaar, Amritsar, chapa ya pili

# Neno la Mwenezi

Hii ndiyo tafsiri ya kijitabu 'Mahmood ki Amin' – Amin ya Mahmood. Amin maana yake ni: Ee Mungu Unipokelee dua yangu. Neno Amin pia linamaanisha ile sherehe inayofanywa anapohitimu mtu Kurani Tukufu. Katika tafrija hii shairi lenye maombi kwa aliyehitimu na wengineo linasomwa. (Firozul-Lughaat).

Hadhrat Mirza Bashir-ud-Deen Mahmood Ahmad mwanaye Hadhrat Ahmad[as], alipohitimu mara ya kwanza Kurani Tukufu katika umri wa miaka minane, tafrija moja iliandaliwa na Seyidna Ahmad[as] mnamo Juni 1897 kwa furaha ya mtima. Ndugu toka nje ya Qadian pia walishiriki. Waliohudhuria wote walikaribishwa kwenye chakula kizuri sana. Kwa ajili ya sherehe hii, Seyidna Ahmad[as] alitunga shairi maalum ambalo lilisomwa mbele ya ndugu waliohudhuria. Shairi hili limejaa maombi yaliyoombwa kwa uchungu wa moyo.

Hadhrat Mahmood ndiye Muslih Mau'udi aliyezaliwa sawa na bishara aliyopata Seyidna Ahmad[as] toka kwa Mwenyezi Mungu, na ndiye alikuwa Khalifatul-Masihi II.

Kabla ya shairi lenyewe kuhusu Mahmood kuitimu Kurani Tukufu, mashairi mawili ya Seyidna Ahmad[as] kwa kuisifu Kurani Tukufu yametangulizwa. Na baada ya shairi hili maalumu, zipo beti chache za Hafidh Ahmadullah Khan kuisifu Kurani Tukufu.

Nilijaribu kutoa tafsiri kwa kulingana na maneno ya Kiurdu. Sheikh Ansar Hussain alipanga herufi zake kwa kompyuta na kutayarisha fomati. Mwenyezi Mungu Awajaalie wasomaji kunufaika na kazi hii ya Dawati la Kiswahili.

Jamil R. Rafiq
Wakilut-Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 09 Marchi 2021

**Wimbo wa upendo wa Kurani Tukufu, na kueleza kwamba hakuna budi tofauti bayana iwepo baina ya kauli ya Mungu na kauli ya binadamu, kwa hiyo Kurani Tukufu pasipo shaka ni Neno la Mungu.**

———

Jamala na uzuri wa Kurani ni mwanga wa uahi wa kila Mwislamu. Mwezi wa wengine ni ule wa angani, mwezi wetu ni Kurani.

Mithili yake haionekani machoni, tumeishaona kwa kutafakari sana. Kwa nini isiwe ya pekee, kwani ni Neno Tukufu la Rahmani.

Ndani ya kila ibara yake mna ustawi wa kudumu. Uzuri huo haumo ndani ya kiunga chochote, wala hakuna bustani kama hii.

Hakuna kilicho sawa na Neno Tukufu la Mungu, hata kama ni lulu ya Aman au ni yakuti ya Badakhshan.

Kauli ya binadamu yawezaje kuwa sawa na kauli ya Mungu; huko kuna nguvu ya Kiungu, na huku ufefe – ni tofauti bayana fika.

Yule Ambaye mbele yake malaika wanakiri hawana elimu, binadamu awezaje kuthubutu kuwa sawa Naye katika umbuji!

Binadamu hawezi katu kutengeneza hata mguu wa sisimizi; itawezaje rahisi kwake kutengeneza nuru ya haki.

Enyi watu, iheshimuni shani ya Mtukufu; nyamazeni kimya hata sasa, kama mnayo imani kidogo.

Kumfanya aliye ghairi ya Mungu kuwa sawa na Mungu ni kufuru kubwa. Mcheni Mungu kidogo, Enyi marafiki; ni uongo gani huu na masingizio!

Kama mnamkiri Mungu Mmoja, kwa nini moyoni mwenu mmefichika ushirikina mwingi kiasi hiki.

Yalifunikaje nyoyo zenu mapazia haya ya ujahili! Mnafanya uhalifu; jizuieni kama mnayo hofu kidogo ya Mungu.

Enyi ndugu, hatuna inadi hata kidogo; ni nasaha kwa unyenyekevu. Kama mtu awe ametakasika moyo wake, twajitolea kwake moyo na uhai wetu.

## Wimbo Mwingine

Nuru ya Furkani ikathibitika kuwa na mng'ao mkali kuliko nuru zote. Yu Mtakatifu ulimotokeza mto huu wa miangaza.

Mmea wa Tauhidi ya Mungu ulikuwa karibu kunyauka; ghafula ikatokeza toka kwa ghaibu chemchem hii safi kabisa.

Ee Mungu! Furkani yako ndio ulimwengu mzima; chochote kilichokuwa cha lazima kimepatikana ndani mwake.

Tumeishachunguza dunia nzima, takaangalia maduka yote; chupa ya divai ya maarifa [ya Mungu] ikathibitika hii hii moja tu.

Yawezaje duniani kuwa tashbihi ya nuru hii; hii ikatokeza ya pekee katika kila jambo na kila sifa.

Kwanza tulifikiri kwamba Furkan ndiyo fimbo ya Musa; kisha tulipotafakari tukatambua kuwa kila neno lake ni Masiya.

Ni kasoro ya vipofu wenyewe, waila nuru hii ikang'ara kiasi hiki kwamba ikawa sawa na majua mia yang'aayo.

Maisha ya wale humu duniani ni bure kabisa, ambao juu ya uwepo wa nuru hii moyo wao bado umepofuka.

Watu hawa wanaungua kabla ya kuchomwa na wivu, ambao kila walisemalo likathibitika kuwa uongo mtupu.

## Amin ya Mahmood

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ[1]

نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّيْ عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ[2]

Hamdu na sifa zote njema zamhusu Yule Aliye Mzima wa milele. Hakuna aliye sawa naye wala hakuna mwenzi wake.
Ni Yeye tu atakayebaki milele, wengine wote minghairi yake watatoweka; kuwapenda wengine minghairi yake ni kisa cha uongo.
Wote ni wageni tu; Yeye ndiye Mwandani pekee. Moyoni mwangu ndimo: Namtukuza Yule Anionaye.

Yu Mtukufu, nguvu yake i tukufu; adhama yake ndiyo adhama hasa. Waliomkurubia hutetemeka; malaika huingiwa na hofu.
Rehema yake ni kwa wote, twawezaje kumshukuru barabara kwa neema yake. Sisi sote ni viumbe wake, basi Mpendeni Yeye tu.
Ghera yake yawezaje kupenda kuwa watu waingiwe na huba ya wengine. Ibariki siku hii; namtukuza Anionaye.

Raha yoyote tuliyonayo ni ukarimu na hisani yake. Tumemuuzia mtima; mtimani mna adhama Yake.
Ni afadhali kumtii Yeye; ndani mwa utii mna bahati njema. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema na ukarimu.
[2] Twamhimidia Yeye, na kumsalia Mtume Wake mhashamu.

Yu tegemeo la wote, Rehema yake i wazi fika. Yu pekee mpendwa wetu; Yu pekee muhibu wetu.
Hatujiwezi pasipo Yeye, kila kitu minghairi yake ni uongo. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Mola, ni hisani Yako, najitolea kizingitini pako. Umetupatia imani; U Mlinzi wakati wote.
Ukarimu wako twaupata kila saa. U Mwingi wa ukarimu, Mwingi wa rehema. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Yawezekanaje kutoa shukurani yake barabara; ni chako kilicho changu. Umejaza nyumba yangu kwa ukarimu wako.
Ulipokuja mwanga wako, kiza kikatoweka. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Wewe Umenionyesha siku hii ambapo Mahmood amekuja akishahitimu. Kwa kuona hisani hii, moyo ukaimba kwa kukusifu:
Ee Mungu, nakutolea shukurani mara mia; nakutolea shukurani mara mia, Ee Mungu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Kwawezaje kukutolea shukurani barabara, Ee Mtunzi wa mtumishi. Wewe Umenipa hawa watumishi wako watatu.
Mimi ni Wako tu kabisa, U Mola wangu Mkuu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Leo Kurani imehitimika, yametimia niliyotamani. Umenionyesha siku hii, najitolea Kwako.
Mola Mhisani wangu, iwezeje shukurani barabara kwa hisani Yako. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Hii yote ni ukarimu Wako; U Rehema timilifu. Nawezaje kukuhimidia sawasawa. Kalamu haina uwezo huu. Ni Wako mie, maadamu navuta pumzi. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Ewe Mweza, Mwenye nguvu, Utulinde na maafa. Tumefika mlangoni pako; tumekuamini. Moyo hauna haja ya wengine tangu nilipokutambua. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Muhibu wangu, Usiwe kuniweka mimi niliye hakiri mbali Nawe; ni afadhali kufa karibu nawe kuliko kuishi [mbali nawe]. Wallahi, ni afadhali kupatwa na huzuni kwa ajili yako kuliko kupata furaha. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Kazi zote Umenifanyia; wana pia nimejaaliwa toka kwako. Yote ni ukarimu Wako; hatukuleta chochote toka nyumbani mwetu. Ee Mpendwa wangu, Wewe tu Umenionyesha siku za fuaha. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Wanangu hawa watatu ni matunda, Ulionijaalia. Hawa ndio wazao wangu walio watumwa wa mlangoni pako.

U Mwenye kutimiza ahadi zako; wakanao wako wapi? Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Uwajaalie bahati njema; Uwape dini na utajiri. Uwahifadhi Wewe Mwenyewe; rehema Yako iwe juu yao. Uwape mwongozo na hidaya, umuri na heshima. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Ewe Mtunzi wangu mie mtumwa wako, Uwajaalie kuwa wenye bahati njema; wawe wenye daraja ya juu, na Uwatunukie taji na tuzo. U Mwongozi wetu, hakuna aliye sawa Nawe. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Waweke mbali ni shetani; Uwajaalie ukaribu Wako. Uijaze roho nuru, na moyo Uujaze sururi. Nijitolee Kwako, Uwajaalie rehema Yako. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Ewe Mwumbaji, nipokelee dua zangu zote. Nijitolee kwako, Utuletee msaada Wako. Tumefika mlangoni pako kwa matarajio makubwa sana. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Mahmood, mtoto wangu mpendwa, yu mtumishi Wako; Umpe dini na utajiri, Uondolee mbali kila giza. Siku ziwe zenye kutimiza matarajio; macheo yawe yamejaa mwangaza. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Yeye anao ndugu wawili, waweke katika hali njema sana – Wako Bashir Ahmad, Wako Sharif yule mdogo. Wote uwape fadhili sana, Wafiridishe kwa rehema. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Hawa wote watatu ni watumishi wako; Usiwaache wawe wachafu. Vishawishi vyote vya dunia viweke mbali nao. Wadumu kuwe wema, Usiwaache wawe walegevu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Ewe Mpenzi Wangu wa moyo, Ee Mkarimu wetu, uwang'arishe kama zilivyo nyota. Uwafanyie fadhili, wote wawe wema na johari. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Ewe Muhibu wangu wa moyo, Ee Mfalme wa dunia na Akhera, Ufanye fadhili hii kwamba asiwepo aliye sawa nao. Wape bahati njema ya kudumu na baraka ya kimbingu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Ewe Mungu wangu Mpendwa, sikiliza maombi yangu yote, nijitolee kwako, waweke kwa rehema yako. Waweke ndani ya hifadhi Yako kwa kusikia kilio changu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Ewe Uliye Mmoja na wa Pekee, Ewe Muumba wa zama, nipokelee dua zangu na maombi ya mtumishi. Nawatolea Kwako wote watatu, wafanye mwezi wa dini. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Moyo una huzuni kwa fikara nyingi, roho yasumbuka. Ule uwezo wa subira niliokuwa nao, sinao sasa. Uweke mbali na kila ghamu, U Mola wa walimwengu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Uzidishe bahati njema, sasa Utuletee fadhili. Tukinge na kila huzuni; tuokoe katika kila udhia. Mwenyewe Utekeleza kazi zangu; Ee Mola, Usinijaribu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Watumishi wako hawa watatu wawe wenye kuiongoza dunia, wawe waongozi wa dunia, wawe nuru fika. Hawa wawe wanaendewa na wafalme, nao wawe jua lenye miangaza. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Wawe wenye heshima, fahari ya maeneo. Wajitolee kwa haki, wawe marafiki wa Mola. Wastawi sana. Kila mmoja abarikiwe kuwa elfu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Ni Wewe tu ndiwe Hulea na kutunza kila saa, Unaondolea mbali huzuni na kukinga na maumivu. Unazitakasa nyoyo, na kutilia haki moyoni. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Wewe Umetufundisha Kurani iliyo msingi wa imani, itoayo maarifa na kufukuza shetani. Hii yote ndiyo hisani Yako; nijitolee Kwako uhai. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Nabii Wako aliyekuja, ametuonyesha Mungu. Akaleta dini imara na kufuta bidaa zote. Akaita kwenye haki akatukutanisha na Mungu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Wote walio wapendwa wangu wanajitolea kwako. Hisani Zako ni kubwa, nasi tumeshindwa kwa kuzihesabu. Nyoyo zahuzunika kwa ghamu; Yafikishe mashua pwani. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Mtimani humu mna nyumba yako, nakuangalia Wewe. Nimeangazwa nawe; U mwezi wangu. Nakutegemea Wewe; kizingitini pako pana hiki kichwa. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Nilipokupenda sana, nikavumilia udhia mwingi, nimejitilifikisha mwili; uhai wangu ukapatwa na taabu. Lakini nashukuru nikakupata kwa kupoteza uhai wangu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Wamekuja marafiki wote, Umetuonyesha siku kama hizi; ukarimu Wako Umewaleta hawa wenye moyo wa kupenda. Siku hii yenye baraka imetokeza ambamo tumepata makusudio yetu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Wageni kwa sababu ya kupendana walipokuja kwa upendo sana, moyo wangu umefurahi na nimepata raha mtimani. Lakini nilihuzunika moyoni nilipowakumbuka

wakati wa kuaga. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Dunia pia ni nyumba ya mapamziko kwa wasafiri; atakayeonana, hakuna budi ataachana. Hata kama ameishi miaka mia, hatimaye atatengana. Hakuna maana kulalamika, kwani nyumba hii yenyewe ni ya kutoweka. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Enyi marafiki, wapendwa! Msiisahau Akhera; Chukueni masurufu kidogo, pitisheni muda kidogo katika matendo mema. Dunia ni mahali pa kutoweka, iondoleeni mbali mtimani. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Msiwe na upendo wake; uachisheni moyo nayo; msielekee kwake; mjitenge mbali nayo. Enyi marafiki, hii ndiyo chatu, mjilinde naye. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Kurani Kitabu cha Rahmani, hufundisha njia za maarifa. Ziwe baraka za Mungu juu ya waisomao. Rehema ya Mungu juu yao wanaoiamini. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Hii ndiyo chemchem ya hidaya kwa Yule aliyefadhiliwa. Ni Neno la Mungu hili, kwalo hupatikana Uwalii. Hili lajaalia mwanga mtimani, hupenya moyoni. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

Muwe mnaikumbuka Kurani, na kuwa na itikadi njema. Ikumbukeni Akhera, muwe na masurufu. Ni kiponya maradhi yote, Ewe mpendwa wangu, ushikamane na ukweli na unyofu. Ibariki siku hii; namtukuza Yule Anionaye.

AMIN

## Beti za Bwana Hafidh Ahmadullah Khan

Yule ambaye mdomo wake hutamka Neno la Rahmani, ndani mwa asili yake mmefichika nuru ya Muumbaji.

Ni ajabu kwamba kuna kiherehere cha A, B, C, ilhali lipo Neno la Mungu.

Ndani mwake mmetajwa watu wa zamani na habari za watakaokuja. Katika mabishano, kauli yake ndio uamuzi, kwani hii ndiyo Furkan – yenye kupambanua haki na batili.

Fitina zinapokuwa mfano wa usiku wenye kiza, ndani ya kiza hicho huwa jua liangazalo, mwezi ung'aao.

Hii imewafanya wasioastaarabika wa Uarabuni kuwa wafalme wa zama. Si Bara Arabu tu, fadhili na hisani yake iko juu ya dunia nzima.

Imamu wa zama akafunua mambo ya kweli na maarifa; sasa anashangaa asiyekuwa ameijali Kurani.

Utangulizeni usomaji wake juu ya vitabu vyote, kwani kila heri na baraka imewekwa ndani mwake.

Ametukuka aliyetenda sawa na Kurani; pasi shaka huyo ndiye mtu asifiwaye sana katika dunia na Akhera.

Matatizo yote ya Kurani na Hadithi yanatatuliwa hapa; afike Qadian apendaye kukidhi shauku yake ya mtimani.

**Tangazo la Vitabu**: Ninavyo vitabu vifuatavyo pia kwa kuuza pamwe na kijitabu hiki, ambavyo vinatumwa kwa njia ya V.P., au kwa kuleta bei mapema: Iikadhun Naaimiin, Anna 1; Shahaadatul Kuran, Anna 2; Nurul Kuran, J. 1, Anna 3. Sat Bachan na Aria Dharm vitachapishwa baada ya maombi 50 kufika. Watu 10 wameishaleta maombi.

Mtangazaji:

Dkt. Ibadullah, M. B., Karha Jaimal Singh, Amritsar.